*Mulika, Na. 41 (2), 221-241*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Matumizi ya Kiswahili katika Ujumuishaji wa Kidemokrasia kwenye Uchaguzi Nchini Tanzania

*Fokas Nchimbi*[1]
Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na41t2.7

**Ikisiri**

Makala haya yanaeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ujumuishaji wa kidemokrasia nchini Tanzania kwa kuzingatia matumizi ya lugha hiyo kwenye michakato ya uchaguzi. Lengo la makala haya ni kuonesha maeneo muhimu ya uchaguzi ambamo lugha ya Kiswahili inatumika, na kupendekeza mikakati inayoweza kufanikisha lugha hiyo kutumika zaidi katika masuala ya uchaguzi na kwenye michakato mingine ya ujenzi wa demokrasia Tanzania. Makala haya yanaakisi matumizi na mchango muhimu wa lugha ya Kiswahili katika michakato ya siasa za uchaguzi nchini Tanzania kama sehemu ya ujumuishaji wa kidemokrasia. Inaonesha kuwa katika michakato ya uchaguzi nchini Tanzania, lugha ya Kiswahili inatumiwa ili kufanya mawasiliano yanayoweza kuwajumuisha Watanzania wengi kwenye hatua mbalimbali za shughuli za uchaguzi. Makala haya yanatumia Nadharia ya Uchambuzi Kilongo. Nadharia hii inaeleza kuwa athari za matumizi ya lugha hazibaki kwenye eneo lake la matumizi pekee bali huvuka mipaka ya muktadha wa matumizi yake na kuathiri masilugha mengine. Makala haya yametumia data za upili ambapo nyaraka ngumu na laini zilizoandikwa kwa Kiswahili kuhusu shughuli za uchaguzi nchini Tanzania zilisomwa. Data za utafiti huu zimewasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo ya utafiti uliozaa makala haya yanaonesha kwamba lugha ya Kiswahili inawawezesha Watanzania wengi kujumuishwa kwenye demokrasia ya uchaguzi kupitia michakato mbalimbali ambayo ni uandikaji wa matini tumizi ya uchaguzi, nyimbo za kampeni za uchaguzi, utangazaji wa matokeo ya uchaguzi, uapisho wa viongozi wateule, uandikaji wa ripoti ya uchaguzi na tathmini ya uchaguzi. Makala haya yanapendekeza kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yaimarishwe zaidi kwenye michakato ya uchaguzi na kwenye michakato mingine ya kisiasa ili kujenga ujumuishi mpana wa kidemokrasia.

## 1.0 Utangulizi

Matumizi ya lugha ni muhimu katika ujenzi na ukuzaji wa demokrasia shirikishi. Demokrasia shirikishi ni kipengele kimojawapo cha utawala bora kinachowajumuisha watu wote katika harakati za kupanga, kutekeleza mipango yao, na zaidi ya yote kutathmini na kunufaika na michakato hiyo kwa misingi ya

[1] **Baruapepe:** fokasnchimbi@gmail.com

kuwapo kwa fursa sawa kwa wanajumuiya wote (Mkude, 1999). Ujumuishaji na ushiriki wa jamii pana ya Watanzania katika mradi endelevu wa ujenzi wa demokrasia unawezekana tu kama watu wote hadi kwenye ngazi ya miji midogomidogo, vijiji na vitongoji watajumuishwa na kuwezeshwa kushiriki katika shughuli za kisiasa. Uwezekano huo unaweza kushuhudiwa katika shughuli za kisiasa ikiwa lugha inayotumika katika shughuli hizo inafahamika, inazungumzwa na kutumiwa zaidi miongoni mwa wanajamii siasa husika (Nanyama, 2015). Wanajamii siasa ni jamii ya watu yenye serikali kamili, yaani ni jumla ya wananchi wote katika nchi yenye serikali yake. Makala haya yanazungumzia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ujenzi wa demokrasia jumuishi nchini Tanzania katika mchakato wa uchaguzi.

Uchaguzi ni utaratibu mmojawapo wa kupata uongozi mpya wa kushika ofisi ya umma au kutoa serikali ya zamani katika mfumo wa kisiasa. Serikali ya kuchaguliwa ni chombo kikuu cha uwakilishi cha kidemokrasia ambapo maamuzi ya nani anashika mamlaka ya utungaji wa sheria na mamlaka ya utendaji katika nchi hufanyika (Stafin, 2006). Kwa mujibu wa Lincolin (1860) na Phillips (2012), uchaguzi ni mchakato wa kumchagua mtu ili awawakilishe watu wengine kwenye ofisi ya umma. Lincon anafafanua kuwa uchaguzi ni mchakato wa kumchagua mtu na kumweka kwenye ofisi ya umma au mchakato wa kukataa pendekezo fulani la kisiasa kwa njia ya upigaji kura. Uchaguzi unaweza kuwa jumuishi na shirikishi ikiwa michakato yake muhimu inajumuisha matumizi ya lugha inayofahamika, kuzungumzwa na kutumiwa na watu wengi zaidi katika jamii siasa kama chombo cha mawasiliano na uwezeshaji wa shughuli zote za uchaguzi (Nanyama, 2015).

## 2.0 Methodolojia

Makala haya yametumia data za upili ambapo nyaraka ngumu na laini zilizoandikwa kwa Kiswahili kuhusu shughuli za uchaguzi nchini Tanzania zilisomwa. Nyaraka ngumu zilizosomwa ni pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 hadi 2025 na Taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuhusu uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani wa 2015. Nyaraka laini zilizotumika katika uandikaji wa makala haya zilijumuisha hotuba za uchaguzi kutoka vyama vya siasa vya Chama cha Mapinduzi (CCM), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), chama cha Civic United Front (CUF) pamoja na chama cha Alliance for Change and Transparency – Wazalendo (ACT – Wazalendo), nyimbo za kampeni za uchaguzi, taarifa ya utangazaji matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, maelezo ya uapisho wa viongozi wateule wa urais, ripoti ya mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na ripoti ya tathmini ya mwisho ya uchaguzi. Data za utafiti huu zimewasilishwa kwa njia ya maelezo kwa mfuatano wa matukio katika mchakato mzima wa uchaguzi hususani Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

## 3.0 Nadharia ya Utafiti

Makala haya yametumia Nadharia ya Uchambuzi Kilongo. Kilongo ni dhana inayohusisha muktadha, mazingira na hali fulani ambamo maarifa mahususi huzalishwa na kuwafikia watu wengine. Dhana ya kilongo haihusiki tu na maudhui ya kile kinachosemwa au kuoneshwa (kwa mfano, matini iliyochapwa, mhadhara, hotuba, matangazo, vitu vya kwenye makumbusho, vipindi vya televisheni na kadhalika), bali pia hujumuisha hali za kidhahania, kihistoria, kijamii, kisiasa na kiuchumi zilizojificha katika kauli zinazotolewa katika kilongo husika. Kilongo hukusanya watu, majengo, taasisi, tawala, amali, shauku, dhana, mashine, vyombo na kitu kingine chochote kile kinachoweza kuwa na mchango katika uundaji maarifa. Kilongo pia huhusu ujumuishi na utengaji wa watu. Kwa maneno mengine, inaweza kusemwa kuwa katika utoaji wa kilongo kauli hupangwa kulingana na mifumo ya kijamii ambapo baadhi ya watu hujumuishwa na wengine kutengwa nje; na michango kutoka kwa baadhi ya watu huthibitishwa kuwa halali au kuwa inafaa kwa tathmini ilhali mingine ikihukumiwa kuwa haifai hata kujadiliwa au kutolewa maoni.

Nadharia ya Uchambuzi Kilongo inaeleza kuwa athari za matumizi ya lugha hazibaki kwenye eneo lake la matumizi pekee bali huvuka mipaka ya muktadha wa matumizi yake na kuathiri masilugha mengine. Mwanzilishi wa Nadharia ya Uchambuzi Kilongo ni mwanahistoria na mwanafalsafa wa Kifaransa, Michel Foucault, aliyejihusisha sana na wananadharia ya Umuundo na Baada Umuundo; na hivyo, kuweka msingi kwa wananadharia wengi wa nadharia za kijamii. Mwanafalsafa mwingine anayejinasibisha na Nadharia ya Uchambuzi Kilongo ni Norman Fairclough, Profesa katika Idara ya Isimu na Lugha ya Kiingereza ya Chuo Kikuu cha Lancaster, nchini Uingereza.

Nadharia ya Uchambuzi Kilongo inadai kuwa uchambuzi wa matini au lugha haufanywi kwa ajili yake wenyewe, bali hufanywa kwa ajili ya kupata uthibitisho wa kinadharia kuhusu jinsi lugha inavyofanya kazi katika kushughulikia masuala na changamoto mbalimbali katika jamii. Aidha, Nadharia ya Uchambuzi Kilongo inasema kuwa mara zote tunapotumia lugha ya mazungumzo au maandishi tunajijengea ulimwengu wa shughuli mbalimbali za kibinadamu katika nyanja mbalimbali kama vile katika shughuli za kijamii, kiuchumi na kisiasa (Gee, 1999). Nadharia hii inawawezesha wachambuzi matini kuelewa namna lugha inavyofanya kazi katika utangamano na masilugha mbalimbali kama vile masuala ya kisaikolojia, kijamii, kiutamaduni, kitaasisi, kiuchumi na kisiasa. Kwa maneno mengine, inaweza kusemwa kwamba uelewa tangamani wa lugha husaidia jamii kushughulikia kwa ufanisi matatizo yanayoikabili. Kulingana na Nadharia ya Uchambuzi Kilongo, matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye uchaguzi wa kisiasa hayasaidii tu kufanikishwa michakato ya uchaguzi, bali huenda mbali zaidi kwenye ujenzi wa ujumuishaji wa wadau wengi wa uchaguzi. Matumizi ya lugha ya

Kiswahili katika hatua mbalimbali za michakato ya uchaguzi mkuu wa kisiasa yanawajengea wadau wengi wa uchaguzi uwezo wa uelewa na ushiriki fanisi katika masuala ya uchaguzi. Wadau wengi wa siasa wanazidi kujumuishwa kwenye ujenzi wa demokrasia kadiri lugha ya Kiswahili inavyozidi kutumika kwenye michakato ya uchaguzi.

## 4.0 Ukuzaji wa Demokrasia Jumuishi

Sehemu hii inawasilisha maelezo mafupi kuhusu dhana mbili muhimu. Maelezo ya kwanza yanahusu dhana ya demokrasia kwa ujumla ambapo fasili ya dhana hiyo imetolewa kwa kurejelea maandiko mbalimbali. Pili, kuna maelezo yanayohusu dhana ya ujenzi wa demokrasia ambapo maandiko mbalimbali yamerejelewa.

### 4.1 Demokrasia

Lengo kuu la makala haya si kujadili kwa undani kuhusu fasili mbalimbali za neno demokrasia. Hata hivyo, ili kuweka msingi imara wa maelezo kuhusu dhana ya ujumuishaji wa kidemokrasia kwenye uchaguzi kama kipengele kimojawapo kikuu katika michakato ya ujenzi wa demokrasia ya kisiasa katika Tanzania, hatuna budi angalau kueleza kwa ufupi maana ya jumla ya neno demokrasia. Katika dunia ya kisasa haishangazi kuibuka kwa mijadala kuhusu maana ya demokrasia kwa sababu ya tofauti za viwango na mikabala mbalimbali ya maendeleo ya jamii mbalimbali za hapa ulimwenguni. Kwa hiyo, kupata maana kamili ya neno demokrasia ni kazi ngumu kwa sababu demokrasia ni dhana changamani inayopata maana tofautitofauti katika vipindi mbalimbali vya kihistoria.

Mabadiliko mengi ya dhana ya demokrasia yanatokana na mabadiliko yanayotokea katika jamii na tafsiri mbalimbali za wachambuzi wa mabadiliko hayo na michakato yake. Hata ukiwauliza watu mbalimbali maana ya neno hilo demokrasia, unaweza kupata majibu kuhusu maana yake kutoka kona tofautitofauti kama vile shughuli za kisiasa, haki za binadamu, au shughuli za kijamii na kiraia na huduma za jamii. Watu wengine wanalikabili swali hilo kwa kuorodhesha sifa za jamii siasa wanayofikiri ni ya kidemokrasia kama vile uhuru wa watu kufanya mambo wanavyotaka, kufanya uchaguzi na uzingatiaji wa haki za binadamu katika jamii hiyo. Hali kadhalika, mara nyingi watu wanapojiuliza kama nchi ina demokrasia au la wanaangalia mambo makuu ya viashiria vya kidemokrasia kama vile suala la uchaguzi.

Kwa kuzingatia mtazamo unaojikita kwenye uchaguzi, demokrasia inafafanuliwa kama mfumo wa utawala ambamo raia wote wenye akili timamu hupiga kura katika vipindi maalumu vilivyowekwa kuwachagua viongozi kutoka miongoni mwa wagombea mbalimbali ili watengeneze na kutekeleza sera za nchi (Shively, 2012). Kwa mujibu wa Anil (2009), neno demokrasia linafasiliwa kama utaratibu wa watu unaowekwa na watu wenyewe na kwa manufaa yao wenyewe. Anil anafafanua

kuwa utaratibu huo unatoa fursa nyingi kwa watu za kujishirikisha kwenye michakato ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ili kupanua uwezo wao. Kwa maneno mengine, inaweza kusemwa kuwa demokrasia ni mfumo wa serikali ambamo, kinadharia, watu wenyewe hutawala ama kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, yaani kutawala nchi yao kwa njia ya wawakilishi waliochaguliwa na wananchi wenyewe (Golden, 2005).

### 4.2 Ujenzi wa Demokrasia Jumuishi

Ujenzi wa demokrasia jumuishi ni mchakato wa makusudi wa kisiasa wa ujenzi na matumizi stahiki ya taasisi za kidemokrasia katika jamii siasa ya kidemokrasia (Komba, 1998). Kwa mujibu wa Komba, jamii ya kidemokrasia haina budi kujua jinsi jamii siasa yake inavyoongozwa, maadili stahiki na nyenzo zinazoijenga na kuikomaza demokrasia yake kama vile kuwapo kwa uwazi, haki, uwajibikaji, upatikanaji wa habari, kufanyika kwa uchaguzi wa kidemokrasia kwa kalenda ya uchaguzi inayotabirika na matumizi ya lugha. Demokrasia jumuishi ni mhimili muhimu katika jitihada za wanajamii siasa kujenga na kudumisha utawala bora katika nchi. Katika makala haya imeoneshwa kuwa ujumuishaji wa kidemokrasia kwa wananchi katika michakato ya kisiasa unaweza kufikiwa kwa kiwango stahiki, ikiwa kutakuwapo na hatua za makusudi za kujenga mazingira wezeshi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za kisiasa. Halikadhalika, makala haya yanaonesha uchomozi wa matumizi ya Kiswahili kama lugha ya shughuli za kisiasa, ukijumuishwa uchaguzi, ambao ni kiashiria kimojawapo kikuu cha ujenzi wa demokrasia hapa Tanzania. Lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika kwenye shughuli za kisiasa kuanzia miongo miwili ya mwisho ya utawala wa ukoloni hapa Afrika Mashariki (Mazrui na Mazrui, 1995).

Watu wengi wanafikiri kuwa kufanya chaguzi tu, hasa chaguzi anzilishi, ni ujenzi wa demokrasia. Pia, wengine wanadhani kuwa kufanya uchaguzi ni sawa na kuwa na demokrasia kamili. Kufanya uchaguzi ni kitu kingine na demokrasia kamili ni kitu kingine tofauti. Ni kweli kuwa uchaguzi ni kipengele muhimu na sababishi cha ujenzi wa demokrasia, lakini si kipengele pekee sababishi katika ujenzi wa demokrasia. Kama uchaguzi si huru na wa haki, haidhuru kwa kiwango gani, tunaweza kusema kuwa uchaguzi huo haukuwa wa kidemokrasia kwa kiwango fulani. Hoja hii inaungwa mkono na Lindberg (2006) anaposema kuwa uchaguzi una umuhimu mkubwa katika ujenzi wa demokrasia na kwamba ni mchakato muhimu katika ufikiaji wa utawala wa watu na uchapuzaji wa ujenzi wa demokrasia. Lakini chaguzi zinazofanyika katika nchi na zinazojenga demokrasia hazimaanishi ukamilifu wa mpito wa kuelekea kwenye demokrasia bali zinachapuza tu uliberali na zina nguvu ya kuongeza demokrasia kwenye tawala za kisiasa.

Kwa kuwa katika demokrasia za kisasa si rahisi kwa jamii siasa nzima kushiriki katika kutoa mawazo na kuamua kuhusu masuala yao kwa pamoja, raia katika nchi za Afrika Mashariki hawana budi kukubali kuwakilishwa na watu wachache katika vyombo vya uwakilishi wa kidemokrasia kama vile katika mabunge, mahakama na taasisi nyingine za utetezi wa haki za binadamu. Mambo hayo ni baadhi tu ya vipengele vya demokrasia liberali. Kwa mujibu wa Mukandala (2001), makubaliano hayo yanaonesha kuwa demokrasia liberali ina sifa ya kuwa na utaratibu wa kikatiba, mfumo wa kisiasa unaoruhusu chaguzi shindanishi na zinazofanyika katika mazingira ya haki za kiraia na kisiasa zinazowekwa na kulindwa kwa mujibu wa sheria. Haki hizi ni pamoja na haki na uhuru wa mtu kujieleza, kujumuika, kuamini na kushiriki katika masuala ya kisiasa kwa hiari.

Ujenzi wa demokrasia ni dhana ya kisiasa inayojumuisha michakato mbalimbali ya kujenga demokrasia au utawala bora. Ujenzi wa demokrasia unaweza kusemwa unatokea katika mazingira ya kisiasa ambapo kuna ujenzi wa taasisi za kidemokrasia. Tunaposema ujenzi wa taasisi za kidemokrasia tunamaanisha kuwepo kwa hatua za makusudi za kujenga serikali za kiraia, mabunge ya wananchi, mahakama na vyombo vyake pamoja na michakato ya kudumisha ujenzi wa jamii za kiraia, ushiriki, ushirikishaji na ujishirikishaji, ushindani sawa na wa haki, chaguzi shindanishi za kisiasa, na kadhalika (Bratt na Walle, 1998). Ujenzi wa demokrasia ni dhana na mchakato endelevu wa kisiasa kwa sababu mpaka sasa hakuna nchi ulimwenguni iliyofikia demokrasia kamili. Kwa hiyo, tunasema kuwa udemokrasishaji ni dhana telezi kwa sababu hakuna demokrasia kamili (Mkude, 1999). Ujenzi wa demokrasia ni mchakato usio na ukomo ambao unaruhusu kuwepo kwa mfumo wa kitaasisi ambapo jamii za kiraia zinaweza kupata fursa pana ya uwakilishi na ushiriki wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja katika michakato ya kisiasa. Kwa mujibu wa Mengisteab (1996), ujenzi wa demokrasia ni utaratibu wa jamii wa kuweka mkakati wa makusudi wa kupanga na kutekeleza mpango wa kisiasa unaowawezesha raia katika nchi kuwa na mamlaka ya kufanya maamuzi kila wakati kuhusu masuala muhimu yanayohusu maisha yao. Kuhitimisha sehemu hii, inaweza kusemwa kuwa ujenzi wa demokrasia ni uanzishaji wa taasisi za kidemokrasia na matumizi yake stahiki na endelevu katika shughuli zote za kisiasa katika jamii siasa husika. Ujenzi wa taasisi za kidemokrasia unawawezesha wanajamii siasa kujuuishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja katika vyombo vya majadiliano na maamuzi. Mojawapo ya njia za kuunda taasisi za kidemokrasia katika nchi ni uendeshwaji wa uchaguzi wa kisiasa. Kwa njia ya chaguzi za kisiasa wanajamii siasa wanaweza kuchagua madiwani kuunda mabaraza ya madiwahi katika halmashauri na manispaa, kuchagua wabunge kuunda bunge, kuwachagua rais na makamu wake ili kuunda taasisi ya urais.

## 5.0 Matumizi ya Kiswahili katika uchaguzi

Kiswahili kilitangazwa rasmi kuwa lugha ya taifa nchini Tanzania mnamo mwaka 1962. Lugha hii inafahamika na kuzungumzwa na watu wengi zaidi nchini Tanzania. Tangu zama za harakati za ukombozi kulikuwa na matumizi ya makusudi ya lugha ya Kiswahili ambapo lugha hiyo ilikuwa ni nyenzo muhimu ya ujumuishaji wa wananchi kwenye harakati za ukombozi (Mazrui na Mazrui, 1995). Halikadhalika, katika masuala ya kisiasa ya zama hizi, kuna namna mbalimbali zinazoweza kutumika kujenga ujumuishaji wa kidemokrasia miongoni mwa wanajamii siasa ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha katika uchaguzi. Uchaguzi ni njia mojawapo inayotumika kujenga ujumuishaji wa kidemokrasia.

Suala la umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika ujumuishaji wa kidemokrasia nchini Tanzania linaweza kueleweka vizuri kwa kuchunguza matumizi ya lugha hiyo katika michakato mbalimbali ya kisiasa ikijumuisha michakato ya chaguzi za kisiasa. Katika makala haya tunaonesha matumizi ya Kiswahili katika masuala msingi ya uchaguzi ikichukuliwa kwamba uchaguzi ni kipengele kimojawapo muhimu katika michakato ya ujenzi na ukuzaji wa demokrasia jumuishi. Data za utafiti huu zinaonesha kuwa katika michakato ya uchaguzi lugha ya Kiswahili inatumika kwenye hatua na shughuli mbalimbali. Shughuli hizo zinajumuisha vipengele vikuu vifuatavyo vya uchaguzi: uandikaji wa matini tumizi za uchaguzi (daftari la wapiga kura, fomu za kupigia kura na kanuni za uchaguzi), utoaji wa elimu kwa wapiga kura, utoaji wa hotuba za uchaguzi kutoka kwa wagombea na maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ilani za uchaguzi za vyama mbalimbali vya siasa, utangazaji wa matokeo ya uchaguzi, uapisho wa viongozi teule, uandikaji wa ripoti ya uchaguzi na uandikaji wa tathmini ya uchaguzi. Kufuatana na Nadharia ya Uchambuzi Kilongo, dhima ya lugha ya Kiswahili haiishi tu kwenye kufanikisha shughuli za uchaguzi, bali huchagia kwenye ujenzi wa demokrasia jumuishi.

### 5.1 Kiswahili katika Uandikaji wa Matini Tumizi za Uchaguzi

Uchaguzi wa kisiasa ni mchakato unaohitaji matumizi ya rasilimali nyingi kama vile vifaa vya uchaguzi. Mojawapo ya vifaa vinavyotumiwa kwenye zoezi la uchaguzi ni matini mbalimbali za uchaguzi zinazojumuisha daftari la wapiga kura, kanuni za uchaguzi na fomu za kupigia kura. Data zilizokusanywa katika kufanya uchunguzi huu zinaonesha kuwa lugha ya Kiswahili inatumika katika maelezo kuhusu uboreshaji wa taarifa za mpiga kura kwenye daftari la wapiga kura ili kuwawezesha walengwa kuelewa vema mchakato wa zoezi la uboreshaji wa daftari hilo. Rejea Data Na. 1 hapa chini:

1. Ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeipa Tume jukumu la kusimamia na kuratibu uandikishaji wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani katika Jamhuri ya Muungano. Zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura ni sehemu muhimu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba 2020. Uboreshaji wa daftari hilo ulihusisha shughuli kuu nne,

> uandikishaji wapiga kura wapya ambao wametimiza umri wa miaka 18 na wengine ambao watafikisha umri huo mwezi Oktoba. Ulihusisha pia watu ambao wamehamia maeneo mengine ya makazi na walipenda kuhamishia taarifa zao huko. Zoezi hili lilitoa fursa kwa wapiga kura ambao vitambulisho vyao vimeharibika au kupotea kupata vitambulisho vipya. Mwisho, zoezi la kuandikisha wapiga kura lilihusisha kuwaondoa kutoka kwenye daftari la kudumu la wapiga kura watu waliopoteza sifa za kuwa wapiga kura, kama watu waliofariki.
> **Chanzo:** TEMCO (2020)

Matini katika Data Na. 1 inadhihirisha matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye hatua mbalimbali za mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ambapo wananchi walijiandaa kumchagua rais, wabunge na madiwani. Jukumu mojawapo la Tume ya Taifa ya Uchaguzi nchini Tanzania ni kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura. Taarifa za awali kuhusu zoezi la uboresahji wa daftari la kudumu la wapiga kura zinatolewa na Kamati ya Uangalizi wa Uchaguzi Tanzania (TEMCO) kwa lugha ya Kiswahili. Pamoja na kuchangia kwenye uandikaji wa daftari la kudumu la wapiga kura na uandikaji wa taarifa zinalolihusu daftari hilo, matumizi ya lugha ya Kiswahili yana mchango mkubwa kwenye suala la ujenzi wa ujumuishaji wa kidemokrasia.

### 5.2 Kiswahili katika Utoaji wa Elimu kwa Mpiga Kura

Elimu ya mpiga kura ni muhimu kwa ajili ya kuwaelimisha wapiga kura kuhusu umuhimu na namna ya kutumia haki yao ya kikatiba na kuhamasihwa kushiriki katika mchakato wa uchaguzi ili kutuma haki hiyo ya kikatiba ya kupiga kura kwa usahihi na ukamilifu (Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2015). Kwa mujibu wa Kifungu cha 4C cha sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 utoaji wa elimu ya mpiga kura ni mojawapo ya majukumu ya lazima ya Tume ya Uchaguzi. Ili kuwawezesha raia wengi kupata elimu hiyo ya mpiga kura, lugha ya Kiswahili inatumika kutoa maudhui kama inavyoonekana katika Data.Na. 2 a-c.

2. (a*) Awe amejiandikisha katika Daftari la kudumu la wapiga kura:*
   *(b) Awe ana Kadi ya Mpiga Kura iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi;*
   *(c) Awe katika kituo alichojiandikisha kupiga kura*
   **Chanzo:** https://www.nec.go.tz/howdo/6

Katika Data Na. 2 (a), (b) na (c) kuna vipengele vinavyoonesha masharti yanayopaswa kutimizwa na raia wa Tanzania mwenye haki ya kupiga kura. Masharti hayo yanaonesha kuwa pamoja na raia wa Tanzania kuwa na haki ya kupiga kura kwa kutimiza vigezo vingine kama vile kuwa na umri wa kuanzia miaka 18 umri na kuwa raia mwenye akili timamu, mpiga kura anatakiwa kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la mpiga kura, kuwa na kadi ya mpiga kura ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kupiga kura kwenye kituo alichojiandikisha

isipokuwa kwa uchaguzi wa urais. Katika uchaguzi wa urais mpiga kura aliyejiandikisha anaweza kupiga kura yake kituo chochote ilimradi awe amejiandikisha na kuwasilisha kitambulisho chake kwa msimamizi wa kituo. Matumizi ya Kiswahili katika utoaji wa elimu hiyo ya mpiga kura yanawawezesha wananchi wengi kuelewa masharti yanayotolewa na hivyo kujumuishwa zaidi kidemokrasia katika mchakato wa uchaguzi.

**5.3 Kiswahili katika Ilani za Uchaguzi za Vyama vya Siasa**

Ilani ya uchaguzi ni maelezo ya chama kuhusu sera, mikakati na mipango ambayo chama cha siasa kinakusudia kutekeleza katika kipindi fulani ikiwa kinachaguliwa kuongoza dola katika nchi. Wakati wa kampeni za uchaguzi kila chama cha kisiasa kinachogombania nafasi za uongozi kinakuwa na ilani yake ya uchaguzi. Nchini Tanzania ilani za vyama vya siasa huandikwa kwa Kiswahili ili wananchi wengi wapate kuelewa na hivyo kujumuishwa kidemokrasia kwa ufanisi zaidi. Data Na. 3 inayofuata inawasilisha sehemu ndogo ya matini ya ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 hadi 2025.

3 … CCM inaamini pia kuwa kila mtu ana jukumu la kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kujiletea maendeleo yake na Taifa kwa ujumla. Imani hii ndiyo chimbuko la kauli mbiu za Hapa Kazi Tu! na Kuacha Kufanya Kazi kwa Mazoea! Aidha, CCM inatambua kuwa serikali inazoziongoza zina jukumu la msingi la kuhakikisha kuwa walio wanyonge katika jamii wanapata fursa ya kipekee ya kustawisha maisha yao na kuondokana na unyonge wao ili kupunguza tofauti za matabaka ... CCM itahakikisha serikali zake zinatekeleza mambo yote yaliyoahidiwa katika Ilani hii kwa manufaa na ustawi wa Taifa letu. Utekelezaji wa Ilani hii utaongozwa na kauli mbiu ifuatayo: "Tumetekeleza kwa Kishindo; Tunasonga Mbele Pamoja" 11. Ilani hii ni tamko na ahadi maalumu ya nia inayodhihirisha uwezo wa CCM kuendelea kuongoza nchi, kuleta ustawi wa Watanzania wote na kuendelea kutatua changamoto zinazowakabili wananchi, hususan wanawake, vijana, watoto, wazee, pamoja na watu wenye ulemavu. Katika miaka mitano ijayo, CCM itahakikisha matarajio ya wananchi katika nyanja zote yanafikiwa. Chama Cha Mapinduzi kinawaomba Watanzania wote waendelee kukiamini na kukichagua ili kiendelee kuongoza nchi na kuleta maendeleo makubwa na ya haraka kwa faida ya wananchi wote.

**Chanzo:** Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM (2020: 1)

Sehemu hii ya ilani ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025 inafanya kampeni kwa kuonesha umuhimu wa kila raia kufanya kazi kwa maneno 'Hapa Kazi Tu'. Pia, sehemu hii ya ilani inaeleza azma ya CCM ya kuweka mikakati ya makusudi ya kuwainua wanyonge ili kuondoa unyonge na kupunguza tofauti za kitabaka baina ya walionacho na wasionacho. Halikadhalika, sehemu hii ya ilani inanadi kaulimbiu ya kampeni za uchaguzi za CCM ambayo ni *"Tumetekeleza kwa Kishindo; Tunasonga Mbele Pamoja"*. Maelezo hayo pamoja na kaulimbiu vinapowasilishwa

kwa lugha ya Kiswahili vinawezesha ujumuishwaji fanisi wa wanajamii siasa kwenye michakato ya uchaguzi na mchakato mkuu wa ujenzi wa demokrasia. Mchakato wa kidemokrasia wa uchaguzi unakuwa fanisi na jumuishi zaidi katika jamii siasa ya Watanzania kwa kuhusisha matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Halikadhalika, Data Na. 4 inayofuata inawasilisha sehemu ndogo ya matini ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ya mwaka 2020 hadi 2025 iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

4. … Ibara ya 4.1.4 ya Katiba ya CHADEMA inatamka madhumuni ya CHADEMA kuwa ni: "Kuendeleza na kudumisha Demokrasia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, kujenga utamaduni wa demokrasia katika jamii kwa kutambua haki za wengi katika maamuzi; na pia kutambua haki za wachache kusikilizwa, kuheshimiwa na kulindwa, sambamba na kukubali ushindani huru, wa haki na wa wazi katika uchaguzi… Falsafa hii na madhumuni haya ya CHADEMA ni mwendelezo na maboresho ya falsafa na madhumuni yaliyoongoza juhudi za Watanzania kupigania uhuru wao toka kwa wakoloni. Juhudi hizi zilikuwa ni kiini cha ukombozi wa awamu ya kwanza wa Tanzania. Miaka kadhaa baada ya ukombozi wa awamu ya kwanza Watanzania wamejikuta wakihitaji ukombozi wa awamu ya pili. Ukombozi huu wa awamu ya pili unasukumwa na falsafa na madhumuni yanayofanana kwa vile, yanalenga kumtoa Mtanzania katika hali duni kwenda kwenye hali bora zaidi ya maisha.'

   **Chanzo:** UNIFORUMTZ.%20COM_CHADEMA%20(2).pdf

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, CHADEMA ambacho wakati wa uchaguzi huo kilikuwa chama kikuu cha upinzani nchini Tanzania, kiliandika ilani yake katika lugha ya Kiswahili. Sehemu ya matini ya ilani hiyo iliyowasilishwa kwenye Data Na. 4 inanadi sera ya CHADEMA ya kuendeleza na kudumisha Demokrasia ya mfumo wa vyama vingi, kujenga utamaduni wa demokrasia katika jamii kwa kutambua haki za wengi katika maamuzi; na pia kutambua haki za wachache kusikilizwa, kuheshimiwa na kulindwa, sambamba na kukubali ushindani huru, wa haki na wa wazi katika uchaguzi. Aidha, matini hii inaonesha msimamo wa CHADEMA kuwa Watanzania wanahitaji ukombozi wa pili wa kumtoa Mtanzania kwenye hali duni kwenda kwenye hali bora zaidi ya maisha.

### 5.4 Kiswahili katika Hotuba za Uchaguzi

Eneo lingine muhimu katika mchakato wa uchaguzi ni kampeni zinazosheheni hotuba mbalimbali zinazotolewa kwa lugha ya Kiswahili. Kampeni za uchaguzi ni zoezi muhimu katika mchakato wa kuelekea kwenye uchaguzi wowote wa kisiasa. Wagombea wa uchaguzi au mawakala wao huendesha kampeni za aina mbalimbali za uchaguzi kama vile kampeni za nyumba kwa nyumba, kampeni za matangazo kupitia vyombo vya habari, mabango na mikutano ya hadhara (Tume ya Uchaguzi,

2015: 51). Kampeni za uchaguzi zinatumika kuelezea ilani na ajenda za vyama mbalimbali ili wananchi wazielewe na kuvutiwa kupigia kura chama wanachoona kina sera na ajenda wanazoweza kunufaika nazo. Hotuba kuhusu masuala ya uchaguzi zinaweza kugawanywa kwenye makundi makuu mawili ambayo ni hotuba za wagombea katika kampeni za uchaguzi na hotuba za maelekezo ya viongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Wakati wa msimu wa uchaguzi wa kisiasa hotuba nyingi hutolewa na wanasiasa lugha ya Kiswahili inatumiwa na wagombea na wapambe au mawakala wao kwenye mikutano mbalimbali ya hadhara ya kampeni za uchaguzi. Data za utafiti huu zinaonesha kuwa katika kampeni za uchaguzi wa Mkuu wa Mwaka 2020 wagombea wa uchaguzi huo katika ngazi ya urais walitumia lugha ya Kiswahili katika kunadi ilani na sera zao kwa wananchi wapiga kura. Katika mkutano wa ufunguzi wa kampeni za CCM jijini Dodoma tarehe 29 Septemba 2020 mgombea wa urais wa chama hicho, hayati John Joseph Magufuli aliwahutubia wananchi kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Data Na. 5 inadhihirisha matumizi ya Kiswahili kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania, kama ifuatavyo:

5. Mimi na wenzangu katika Chama cha Mapinduzi tunaamini tumejitahidi yale tuliyoweza ndani ya kipindi cha miaka mitano. Tunajua tumejenga misingi mikubwa. Tunajua kwamba miradi mikubwa tumeianzisha ambayo sina uhakika kama mkichagua zaidi ya CCM kama watakuja kuiendeleza hiyo mipango… Tupeni kura ndugu zangu. Ninawaomba wana Dodoma mtupe kura kweli kweli. Muwape kura wabunge wangu ili waje wanipitishie bajeti ya mipango mikubwa ambayo tumepanga. Hivyo, ninawaomba Watanzania na Mungu akawajalie. Watanzania wa vyama vyote na hasa kwa sababu maendeleo hayana chama. Maendeleo tunayahitaji sisi Watanzania wote kwa pamoja. Na mimi natambua ndani ya dhamira ya moyo wangu, nimejitoa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa hili na ninatambua kabisa wabunge tuliowapitisha kuwania nafasi mbalimbali za ubunge ni wale ambao watalivusha taifa hili. Ninatambua Madiwani waliopitishwa katika maeneo mbalimbali ni wale madiwani ambao wana lengo la kutekeleza maendeleo ya taifa hili. Ninafahamu pia kwa upande wa Zanzibar tumemchagua Mwinyi… Ni kijana mwenye moyo mzuri. Na ndio maana siku zote nimesema huyu ataisaidia Zanzibar kwa sababu ni mtu ambaye anajituma, ana upendo, hana jazba… Ninawashukuru sana… CCM Oyeeeeh? Tanzania Oyeeeeh? ….”
   **Chanzo:** youtube.com/watch?v=lqtSscGuVc

Data Na. 5 inawasilisha sehemu ya hotuba ya ufunguzi wa kampeni katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 mjini Dodoma tarehe 29 Agosti 2020. Umati wa wananchi waliokusanyika kwenye uwanja wa Jamhuri walimsikiliza mgombea wa nafasi ya urais kutoka CCM, hayati John Pombe Joseph Magufuli akihutubia na kunadi sera zake kwa lugha ya Kiswahili. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yanawezesha wananchi wengi kuelewa maudhui yanayobebwa kwenye hotuba ya

mgombea. Upana wa uelewa kuhusu maudhui ya hotuba za kampeni unalifanya zoezi la uchaguzi kuwa la kidemokrasia na lenye ujumuishi mpana.

Halikadhalika, katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 chama cha upinzani cha CUF kilizindua kampeni zake mjini Mtwara. Mwenyekiti na mgombea wa kiti cha urais wa chama hicho Profesa Ibrahim Lipumba alitoa hotuba yake ya ufunguzi akielezea masuala ya uchumi na ustawi wa jamii. Hotuba yake imetolewa kwa lugha ya Kiswahili kama inavyowasilishwa kwenye Data Na. 6.
Mfano:

6. … Sera ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara. Sera ya kuboresha mazingira ya uwekezaji. Sera ya kuboresha mazingira ya ujasiriamali. Katika kipindi cha miaka mitano mzunguko wa fedha ulikuwa mdogo… hakuna mzunguko unaokidhi mahitaji… Tunahitaji kuibadilisha hali hiyo… kuhakikisha kwamba ujazi wa fedha unakidhi mahitaji. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ujazo wa fedha umeongezeka kwa chini ya asilimia tano. Tunahitaji kuwa na lengo la kukuza uchumi huu uweze kuongeza ajira alau kila mwaka, uchumi, pato la taifa liweze kukuakwa asilimia kumi. Ndugu zangu hilo linawezekana. Ndugu zangu tunaweza kubadilisha hali watu wakawekeza katika maeneo mbalimbali. Uwekezaji wa ndani na uwekezaji wan je. Ndugu zangu ili tuweze kuendelea; tuwe na maendeleo ya muda mrefu, lazima tuwekeze kwa akina mama wajawazito na watoto wachanga… siku elfu moja za mtoto ndio siku muhimu; siku elfu moja za mwanzo. Miezi tisa akiwa katika tumbo la mamake na miaka miwili ndipo mtoto anapojenga kinga ya mwili. Ndipo mtoto anapojenga ubongo wake…

   **Chanzo:** youtube.com/watch?v=JklYigjq_iM

Mtoa hotuba anatumia lugha ya Kiswahili kuwafafanulia wananchi waliohudhuria mkutano wa kampeni masuala ya hali ya uchumi na umuhimu wa sera ya kuwekeza kwa akina mama wajawazito na watoto wachanga. Kwa kutumia uchambuzi wake wa kiuchumi anaeleza kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyotangulia kabla ya kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, kulikuwa na mzunguko mdogo wa fedha na ujazi wa chini wa fedha nchini Tanzania; na hivyo kusababisha mazingira magumu ya biashara, ujasiriamali na uwekezaji wa ndani na nje. Halikadhalika, mtoa hotuba anaeleza kuwa mipango ya maendeleo endelevu ya muda mrefu yanawezekana ikiwa kuna uwekezaji wa makusudi kwa akina mama wajawazito na watoto wachanga. Mambo hayo yote na mengine yanayotolewa kwenye hotuba za kampeni za uchaguzi yanaweza kueleweka vizuri ikiwa lugha inayotumika inafahamika vizuri kwa wasikilizaji. Kwa hiyo, matumizi ya lugha ya Kiswahili yanawezesha usikilizaji na upokeaji wa maudhui ya hotuba za kampeni zinazotolewa na wagombea wa nafasi za uongozi kwenye uchaguzi kwa ufanisi.

Aidha, lugha ya Kiswahili haitumiwi tu na viongozi wagombea wa nafasi ya uongozi kutoka vyama mbalimbali, bali wakati wa mchakato wa uchaguzi Kiswahili hutumiwa na maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutoa taarifa rasmi kwa wasimamizi wa uchaguzi na umma wa Watanzania wote kwa ujumla. Katika kufanya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi alitoa hotuba mbalimbali kwa wadau wa uchaguzi huo. Data Na. 7 ifuatayo inawasilisha matini ya lugha ya Kiswahili inayoonesha sehemu ya hotuba ya Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa wasimamizi wa uchaguzi.

7. "… Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka huu kutakuwa na vituo 81,567 vya kupigia kura kwa nchi nzima. Mmeletewa orodha ya vituo vya kupigia kura vilivyopo katika maeneo yenu. Pia, mmeletewa nakala mbili za orodha za wapiga kura na nakala moja ya daftari la kudumu la wapiga kura kwa kila kituo cha kupigia kura kwa madhumuni ya kutumika katika mchakato wa uchaguzi kama mlivyoelekezwa kwenye mafunzo."

   **Chanzo:** TEMCO (2020)

   Kama mnavyofahamu, kesho tarehe 28 Oktoba, 2020, ni siku ya kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Kwa mujibu wa ibara ya 74(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndicho chombo chenye mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kuendesha uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Tume tayari imekamilisha maandalizi yote muhimu ya uchaguzi, vikiwemo vifaa. Hadi kufikia leo, vifaa vimefikishwa kwenye maeneo husika na sasa zoezi la kusambazwa vifaa hivyo kwenye vituo vya kupigia kura linaendelea. Mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi kwa maana ya wasimamizi wa vituo, wasimamizi wasaidizi na makarani waongozaji wapiga kura yalikamilika tarehe 26 Oktoba, 2020.

   **Chanzo:** Tume ya Taifa ya Uchaguzi (2021)

Matini kwenye Data Na. 7 na Data Na. 8 inaonesha matumizi ya Kiswahili kwenye mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Lugha ya Kiswahili haitumiwi tu na viongozi wagombea kutoka vyama mbalimbali vya siasa kwenye mikutano yao ya kampeni, bali pia hutumiwa na viongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Data Na. 7 ya utafiti inawasilisha matini ya Kiswahili inayohusu sehemu ya hotuba iliyotolewa na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa wasimamizi wakuu wa majimbo mbalimbali ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nchini Tanzania. Halikadhalika, Data Na. 8 inawasilisha hotuba ya Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa wananchi wote wa Tanzania kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye hotuba kama hizo huimarisha ujumuishwaji wa wadau wengi wa uchaguzi na hivyo kuwezesha ujenzi wa demokrasia jumuishi.

### 5.5 Kiswahili katika Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi

Eneo lingine linalodhihirisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika michakato ya uchaguzi nchini Tanzania ni nyimbo. Katika zoezi la kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 wasanii mbalimbali walitunga na kuziwasilisha nyimbo zao za kampeni kwa lugha ya Kiswahili. Lengo kuu la wasanii kutunga na kuimba nyimbo za uchaguzi ni kuwapigia kampeni wagombea wa vyama wanavyojinasibisha navyo katika uchaguzi husika wa kisiasa. Wimbo mmojawapo ulioimbwa kwenye kampeni za CCM katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ni wimbo wa msanii Zuchu anayewasilishwa wimbo wake kwa lugha ya Kiswahili kama inavyooneshwa kwenye Data Na. 8.

8. *We mama njoo. Njoo uone nchi ilivyobadilika*
*Tanzania ya leo imejengwa imejengeka*
*Pita Ubungo Tazara, za juu barabara tayari zinatumika*
*Reli yenye viwango bora standard gauge karibu inakamilikaaa!*

*Tanzania ya sasa mama aiiih mama*
*Ya Magufuli mama aiiih mama*
*Inawakawaka mama aiiih mama*
*Inapendeza sana …*

*Nasema jua lile literemke mama*
*Jua lile literemke mama*
*Wapinzani waterereke sana*
*Wapinzania watetereke…*

*Wazee watoto wanawake hospitali bure*
*Elimu ya msingi pamoja na sekondari bure*
*CCM hai hai hai!*
*Magufuli hai hai hai!*

*Wapinzani wamekaa kaaa!*
*Wamekaa…*
**Chanzo:** youtube.com/watch?v=A9Gf_X0CBs

Msanii anatumia lugha ya Kiswahili kukipigia kampeni Chama cha Mapinduzi na wagombea wake katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 akitaja sifa ya kwamba nchi imebadilika na kupendeza. Anataja baadhi ya mabadiliko hayo kuwa ni pamoja na kujengwa barabara za juu kwenye eneo la Ubungo na TAZARA jijini Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa reli yenye ubora wa kiwango cha juu uliokuwa unaendelea wakati wa kampeni hizo. Jambo lingine analolizungumzia ni utoaji wa baadhi ya huduma za kijamii bila malipo. Huduma anazozataji zinajumuisha matibabu ya bila malipo kwa wazee na watoto pamoja na utoaji wa elimu ya msingi na sekondari bila malipo. Aidha, msanii anawabeza wapinzani wa chama tawala kwa maneno ya ubeti usemao ‘Wapinzani watetereke sana’ na ‘Wapinzania wamekaaa’. Maneno hayo yanamaanisha kuwa wapinzani hawawezi kufua dafu katika uchaguzi huo Mkuu wa Mwaka 2020. Kinyume na maneno hayo ya kubeza

yanayosemwa dhidi ya vyama vya upinzani, msanii anatoa sifa nyingi kwa CCM kuwa chama imara kwa maneno kama 'CCM hai hai hai, Magufuli hai hai hai hai, Dr. Shein hai, Mama Samia hai hai hai…'

Halikadhalika, katika kampeni za chama cha ACT-Wazalendo kulikuwa wimbo uitwao Maalim Seif Shikamoo. Huu ni wimbo mpya wa chama cha ACT – Wazalendo uliotumika kumnadi kiongozi wao hayati Maalim Seif katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Wimbo huo ulioandikwa na kuimbwa kwa lugha ya Kiswahili unawasilishwa kwenye Data Na. 9.

9. *Ulipo tupo baba, Maalim Seif shikamoo!*
*Tuonyesheni mfano ICT tuchagueni.*
*Na hakika Zanzibar Baba Seif hana mpinzani.*
*Hekima busara zake husifika kote duniani.*
*Upole ni ngao yake, nitasema hata hadharani mie.*

*Pita pita Baba Seif uingie ikulu.*
*Sisi sote Zanzibari tuna hamu tuwe huru.*
*Nasema pita iota Baba Seif uingie ikulu*
*Sisi sote Zanzibari tuna hamu tuwe huru*

*Itakuwa busara Baba Seif kumweka kitini.*
*Ataondoa madhara na uovu ulio nchini.*
*Imesimama ishara wananchi wote sikieni.*
*Tumpambe Baba Seif Zanzibar tuwe furahini.*
*Itakuwa busara Baba Seif kumweka kitini.*
**Chanzo:** youtube.com/watch?v=PQp6Obh5d80

Maudhui ya matini kutoka Data Na. 8 ambayo ni sehemu ya wimbo wa chama cha ACT – Wazalendo, inamnadi mgombea wa kiti cha urais tiketi ya chama hicho, hayati Maalim Seif, katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Wimbo huu unaonesha hali ya uungwaji mkono kutoka kwa wanachama wa chama cha ACT – Wazalendo kwa Maalim Seif katika harakati zake za kuusaka urais wa Zanzibar. Aidha, wimbo huo unaorodhesha sifa binafsi za Maalim Seif ambazo ni hekima, busara na upole; zinazosemwa na msanii kuwa zinajulikana duniani kote.

### 5.6 Kiswahili katika Utangazaji wa Matokeo ya Uchaguzi

Utangazaji wa matokeo ni sehemu muhimu katika mchakato wa uchaguzi ambapo mara nyingi hatua hiyo hutarajiwa na kungojewa kwa mshawasha na wadau wote wa uchaguzi. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika utangazaji wa matokeo ya uchaguzi huwawezesha wananchi kufuatilia kwa uelewa wa kutosha hali ya matokeo kwa wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi kama vile udiwani, ubunge na urais. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Mwenyekiti wa Tume ya

Taifa ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza matokeo ya kura za urais kwa lugha ya Kiswahili kama yanavyooneshwa kwenya Data Na. 10.

**Jedwali la Na. 24. Matokeo ya Kura Alizopata kila Mgombea wa Kiti cha Rais**

| Na. | Chama cha Siasa | Jina la Mgombea | Idadi ya Kura | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CCM | Dkt. MAGUFULI John Pombe Joseph | 12,516,252 | 84.40 |
| 2. | NRA | MAHONA Leopold Lucas | 80,787 | 0.54 |
| 3. | ADA-TADEA | SHIBUDA John Paul | 33,086 | 0.22 |
| 4. | SAU | MUTTAMWEGA Bhatt Mgaywa | 14,922 | 0.10 |
| 5. | MAKINI | CECILIA Augustino Mmanga | 14,556 | 0.10 |
| 6. | NCCR - Mageuzi | MAGANJA Yeremia Kulwa | 19,969 | 0.13 |
| 7. | CUF | LIPUMBA Ibrahim Haruna | 72,885 | 0.49 |
| 8. | DP | PHILIPO John Fumbo | 8,283 | 0.06 |
| 9. | ACT-Wazalendo | MEMBE Bernard Kamillius | 81,129 | 0.55 |
| 10. | ADC | QUEEN Cuthbert Sendiga | 7,627 | 0.05 |
| 11. | UPDP | TWALIB Ibrahim Kadege | 6,194 | 0.04 |
| 12. | CHAUMMA | RUNGWE Hashim Spunda | 32,878 | 0.22 |
| 13. | UMD | MAZRUI Khalfani Mohamed | 3,721 | 0.03 |
| 14. | AAFP | SEIF Maalim Seif | 4,635 | 0.03 |
| 15. | CHADEMA | LISSU Tundu Antiphas Mughwai | 1,933,271 | 13.04 |
| **Jumla** | | | 14,830,195 | 100.00 |

**Chanzo:** Tume ya Taifa ya Uchaguzi (2021)

Matini katika Data Na. 10 ni mfano mmojawapo wa utangazaji wa matokeo ya uchaguzi kwa kutumia lugha ya Kiswahili ambapo wadau wengi wa uchaguzi wanaweza kuelewa idadi ya kura zinazotajwa kwa kila mgombea wa nafasi ya uongozi katika uchaguzi huo. Katika data hiyo kuna tangazo linalohusu matokeo ya uchaguzi kwa upande wa wagombea wa kiti cha rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

## 5.7 Kiswahili katika Uapishaji Viongozi Wateule

Kuapishwa kwa viongozi teule wa uchaguzi ni tukio linalohitimisha mchakato mrefu wa uchaguzi wa kisiasa katika nchi. Katika nchi ya Tanzania shughuli hiyo muhimu ya uapishaji wa viongozi wateule hutumia lugha ya Kiswahili. Baada ya kumalizika kwa zoezi la upigaji kura za Uchaguzi Mkuu wa taifa wa Mwaka 2020, uapisho wa rais uliofanyika tarehe 5 Novemba 2020 viongozi wa taasisi ya urais walitoa viapo vyao kwa lugha ya Kiswahili kama inavyowasilishwa kwenye Data Na. 10.

10. ***Katibu Kiongozi:*** *Kiapo cha Rais. Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli*
***Rais Mteule:*** *Mimi John Pombe Joseph Magufuli, naapa kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote; na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.*

*Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.*

*Mimi John Pombe Joseph Magufuli, naapa kwamba nitatenda kazi zangu za urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uaminifu na kutimiza wajibu wa kazi hizo kwa bidii na moyo mkunjufu na kwamba nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa sheria, mila na desturi za Tanzania bila woga, upendeleo, huba wala chuki.*

*Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.*

*Mimi John Pombe Joseph Magufuli, naapa kwamba katika kutekeleza madaraka niliyopewa kwa mujibu wa katiba ya Umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika katiba ya Umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitatetea na kudumisha Umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

*Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.*

**Chanzo**: https://www.google.com/search?q=uapisho+wa+magufuli+2020&oq

Matumizi ya Kiswahili katika kula kiapo cha urais yanawapa wananchi fursa ya kufuatilia hatua za mwisho kabisa za zoezi la Uchaguzi Mkuu. Aidha, wananchi wanawezeshwa kuelewa maudhui ya kiapo cha rais kuhusu wajibu wake kwa katiba, kwa wananchi na kwa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika sehemu ya kwanza ya kiapo cha rais, rais mteule anaapa kuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wake wote. Pia, katika sehemu hiyo ya kwanza ya kiapo hicho, rais mteule anaapa kuihifadhi, kuilinda na kuitetea katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

Sehemu ya pili ya kiapo cha rais inamtaka rais mteule kuapa kwamba atatenda kazi zake za urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uaminifu na kutimiza wajibu wa kazi hizo kwa bidii na moyo mkunjufu. Halikadhalika, rais mteule anaapa kwamba atawatendea haki watu wote kwa mujibu wa sheria; na katika kutekeleza wajibu huo atazingatia mila na desturi za nchi ya Tanzania na kutimiza wajibu wake bila woga, upendeleo, huba wala chuki kwa raia yeyote.

Katika sehemu ya tatu ya kiapo cha rais, rais mteule anaapa kwamba katika kutekeleza madaraka aliyopewa katika katiba ya Umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atawajibika kutetea na kudumisha Umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika uapisho wa urais wa mwaka 2020 makamu wa rais aliapa kwa lugha ya Kiswahili kama inavyowasilishwa katika Data Na. 11.

11. ***Katibu Mkuu Kiongozi:*** *Kiapo cha Makamu wa RaisMheshimiwa Samia Suluhu Hassan*

    ***Makamu wa Rais Mteule:*** *Mimi Samia Suluhu Hassan, naapa kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote; na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.*
    *Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie.*

    *Mimi Samia Suluhu Hassan, naapa kwamba nitaitumikia vema na kwa moyo thabiti Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi yangu ya Makamu wa Rais na kwa wakati wote nitamshauri kwa hekima na uaminifu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa vyovyote vile sitatoa siri ya Baraza la Mawaziri.*

    *Mimi Samia Suluhu Hassan, naapa kwamba katika kutekeleza madaraka niliyopewa kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitatetea na kudumisha Umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*
    *Ee Mwenyezi Mungu nisaidie.*

    **Chanzo:** https://www.google.com/search?q=uapisho+wa+magufuli +2020&oq

Matumizi ya lugha ya Kiswahili yanawawezesha wananchi kuelewa maudhui yaliyomo kwenye kiapo cha makamu wa rais. Maudhui ya sehemu ya kwanza ya kiapo cha makamu wa rais hayatofautiani na maudhui ya sehemu ya kwanza ya kiapo cha rais kwa sababu wote wawili wanaapa kuwa waaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wao wote. Pia, katika sehemu hiyo ya kwanza ya kiapo hicho, Makamu wa Rais mteule anaapa kuihifadhi, kuilinda na kuitetea katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria iliyowekwa.

Maudhui ya kiapo cha makamu wa rais yanatofautiana na yale ya kiapo cha rais kwenye baadhi ya vipengele katika sehemu ya pili. Sehemu ya pili ya kiapo cha makamu wa rais ina maudhui yanayoonesha kuwa mwapaji ataitumikia vema na kwa moyo thabiti Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nafasi ya makamu wa rais. Aidha, makamu wa rais anaapa kwamba atawajibika kumshauri rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hekima na uaminifu; na kwamba kwa namna yoyote hatatoa siri ya baraza la mawaziri. Maudhui ya sehemu ya tatu ya kiapo cha makamu wa rais yanaonesha kuwa muapaji anasema kwamba katika utekelezaji wa majukumu yake kama makamu wa rais ambayo ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atatetea na kudumisha umoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uandikaji na utoaji wa viapo vya viongozi wa taasisi ya urais yanaufanya uapishaji

huo kuwa jumuishi zaidi kwa sababu kwa wananchi wengi, Kiswahili ni lugha yao kuu ya mawasiliano.

### 5.8 Kiswahili katika Taarifa ya Uchaguzi

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa uchaguzi, kazi inayofuata ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni kuandaa taarifa ya uchaguzi na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayekuwapo madarakani wakati huo baada ya uchaguzi na kiapo. Taarifa inayoandaliwa na tume hiyo ya uchaguzi inaelezea namna mchakato wa uchaguzi ulivyoendeshwa na tathmini yake. Matini katika Data Na. 12 inawasilisha mfano mmojawapo wa sehemu ya taarifa kuhusu mwenendo wa uendeshaji wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

12. Tume baada ya kuandaa makisio ya bajeti ya Uchaguzi Mkuu kulingana na mahitaji, ilitengewa jumla ya Shilingi za Tanzania 331,858,287,981.00 kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Wakati wa shughuli za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Tume iliomba na kupatiwa Shilingi za Tanzania 268,493,380,671.00. Kati ya fedha zilizopokelewa, Tume ilitumia Shilingi za Tanzania 262,493,380,671.00 hadi kukamilika kwa zoezi la Uchaguzi Mkuu. Shilingi za Tanzania 6,000,000,000.00 zilibaki na kurejeshwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Gharama za uendeshaji wa uchaguzi zilipungua kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo matumizi ya Mfumo wa Manunuzi wa Kieletroniki - TANePS ambao ulisaidia kuongeza uwazi na ushindani uliopelekea kushuka kwa bei za ununuzi wa vifaa.

Matini hii inaelezea mwenendo wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa lugha ya Kiswahili ambayo inawawezesha wadau wengi wa uchaguzi kuelewa maudhui yake. Sehemu hii ya matini inaeleza kuhusu bajeti ya uchaguzi iliyotengenezwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, pesa zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya uchaguzi na jumla ya fedha iliyotumika kugharimia shughuli za uchaguzi. Kadhalika, matini inawasilisha taarifa kuhusu fedha iliyobaki na kurudishwa kwenye hazina ya serikali baada ya shughuli zote za uchaguzi kukamilika.

## 6.0 Hitimisho

Utawala wa kidemokrasia unaitaka kila jamii siasa iwe na sifa ya kuwepo kwa ushiriki wa umma katika shughuli za kisiasa. Kipengele kimojawapo muhimu cha ushiriki wa kisiasa ni uchaguzi. Uchaguzi ni zoezi linalofanywa na raia wanaostahili kupiga kura kuwachagua wawakilishi wao kwenye ngazi mbalimbali za uongozi katika nchi. Kwa mujibu wa Niyibizi (2011), chaguzi za kisiasa ni barabara muhimu ya kuelekea kwenye demokrasia ya kweli. Ingawa inaweza kuwa vigumu kukubaliana na anachomaanisha kuhusu demokrasia ya kweli, lazima tukubali kuwa, ni kweli kuwa chaguzi zina mchango mkubwa katika ujenzi wa demokrasia jumuishi. Hii ni kwa sababu katika nchi kama Tanzania, chaguzi ndizo zinazounda taasisi za kidemokrasia kama vile bunge, mabaraza ya madiwani na urais. Ushiriki wa wananchi katika siasa nchini Tanzania unaweza kuwa mkubwa, jumuishi na

fanisi zaidi kama matumizi ya lugha ya Kiswahili yanaendelea kuimarishwa kimkakati kwa sababu ndiyo nyenzo muhimu ya kuendesha uchaguzi. Niyibizi (*keshatajwa*), akizungumzia kazi ya kutunga sheria na kanuni za uchaguzi katika nchi ya Rwanda, anaonesha kuwa moja kati ya kanuni zilizowekwa kwa makubaliano ya vyama shiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa ni kuendeshwa kwa njia ambayo iko wazi kwa wananchi wa kawaida. Matumizi ya lugha inayofahamika na wengi ni njia mojawapo ya kufanya uendeshaji wa uchaguzi kuwa wa wazi na jumuishi.

Makala haya yamefafanua matumizi ya lugha ya Kiswahili katika michakato ya chaguzi za kisiasa kama njia mojawapo ya kuufanya ujenzi na uendelezaji wa demokrasia kuwa jumuishi zaidi katika mazingira ya kisiasa ya Tanzania ambamo Kiswahili ni lugha ya taifa. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba katika zoezi la uchaguzi nchini Tanzania, hususani Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, shughuli nyingi zinaendeshwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Shughuli hizo zinajumuisha vipengele vikuu vifuatavyo vya uchaguzi: uandikaji wa matini tumizi za uchaguzi (daftari la wapiga kura, fomu za kupigia kura na kanuni za uchaguzi), utoaji wa elimu kwa wapiga kura, utoaji wa hotuba za uchaguzi kutoka kwa wagombea na maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ilani za uchaguzi za vyama mbalimbali vya siasa, utangazaji wa matokeo ya uchaguzi, kuapishwa kwa viongozi wateule, uandikaji wa ripoti ya uchaguzi pamoja na tathmini ya mwenendo wa uchaguzi.

Pamoja na matumizi makubwa ya lugha ya Kiswahili katika michakato mingi ya uchaguzi, data za utafiti huu zimebaini kuwa bado kuna haja ya kuimarisha matumizi ya lugha hii ya taifa kwenye uandikaji wa kanuni na sheria za uchaguzi. Kwa hiyo, makala haya yanapendekeza kwamba kanuni na sheria za uchaguzi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili kama inavyopendekezwa pia kwenye taarifa ya uchaguzi ya TEMCO kuhusu Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Halikadhalika, kwenye andiko la Taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuna sura mbili zenye mapendekezo ya kutumia lugha ya Kiswahili katika kutafsiri sheria za uchaguzi (Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2021). Katika sura ya nane kuhusu ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi, pendekezo la kwanza la wadau hao linasema sheria za uchaguzi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, katika sura ya kumi na mbili kuhusu hitimisho na mapendekezo katika andiko la tathmini ya uchaguzi iliyofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, pendekezo la kumi na mbili linasema kuwa sheria za uchaguzi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili. Uandikaji wa kanuni na sheria za uchaguzi kwa lugha ya Kiswahili utaongeza viwango vya ujumuishaji wa wadau wa uchaguzi kwa kurahisisha uelewa wa kanuni na sheria husika na kushiriki kwa ufanisi stahiki kwenye michakato ya chaguzi za kisiasa.

## Marejeleo

Anil, K. (2009) *Governance, Democracy and Development*. Delhi: Deep and Deep Publications PVT. LTD.

Bratt, M. na Walle, N. (1998) *Democratic Experiments in Africa: Regime Transitions in Comparative Perspective*. University of Cambridge: Cambridge University Press.

Gee, J.P. (1999) *An Introduction to Discourse Analysis*. London: Routledge.

Golden, J.B. (2005) *The Challenge of Democracy*. New York: Houghton Mifflin Company.

Komba, W.L.M. (1998) "Nafasi ya Elimu ya Msingi katika Ujenzi wa Maadili ya Kidemokrasia Nchini Tanzania". Makala yaliyowasilishwa kwenye Mkutano wa Sita wa Hali ya Siasa Tanzania, Julai 1998.

Lincolin, A. (1860) *The Campain and Election*. Cambridge: Cambridge University Press.

Lindberg, I.S. (2006) *Democracy and Elections in Africa*. Baltimore: The John Hopkins University Press.

Mazrui, A.A. na Mazrui, A.M. (1995) *Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mengisteab, K. (1996) *Globalization and Autocentricity in Africa's Development in the 21st Century Africa*. Asmara: World Press.

Mkude, D.J. (1999) "Ujenzi wa Demokrasia na Sera ya Lugha Nchini Tanzania: Kiswahili/Kiingereza Dhidi ya Lugha za Jamii Ndogondogo". Katika Tumbo-Masabo na Chiduo E.K.F (Wah.) *Kiswahili katika Elimu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Mukandala, S. (2015) "The State and the Provision of Public Services." Katika Mukandala, S. (Mh.) *The Political Economy of Change in Tanzania: Contestations over Identity, the Constitution and Resources*. University of Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Nanyama, D. (2015) "Kiswahili kama Chombo cha Utangamano katika Afrika Mashariki." Katika M. Mukuthuria, J. O. Ontieri, M. Kandagor na S. L. Leo (Wah.) *Kiswahili na Maendeleo ya Jamii*. Dar es Salaam: TATAKI.

Niyibizi, J.M. (2011) "Grassroots Election in Rwanda: The Experience, Challenges and Lessons." Katika *REDET Democratic Transition in East Africa: Governance and Development at the Grassroots*. University of Dar es Salaam: REDET.

Phillips, S.W. (2012) *Power and Choice*. New York: The McGraw-Hill Campanies.

Shively, W.P. (2012) *Power and Choice. An Introduction to Political Science*. New York: The McGraw-Hill Campanies.

Stafin, I. (2006) *Democracy and Election in Africa*. New York: John Hopkins.

TEMCO (2011) *The 2010 Tanzania General Election: Report of the Tanzania Election Monitoring Committee*. Dodoma: TEMCO.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (2015) *Taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani 2015.* Dar es Salaam: Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi. (2021) *Taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani 2020.* Dodoma: Tume ya Taifa ya Uchaguzi.